East African Journal of Swahili Studies
eajss.eanso.org
Volume 4, Issue 1, 2019
ISSN: 1476-4687
EAST AFRICAN NATURE & SCIENCE ORGANIZATION

*Original Article*

# MASIMULIZI KATIKA MCHAKATO WA UFUNDISHAJI WA KIPENGELE MAALUM CHA MSUKO KATIKA RIWAYA YA KIDAGAA KIMEMWOZEA NA ILE YA CHOZI LA HERI.

*Stephen Muyundo Ndinyo[1]*, Dkt. Fred Simiyu[2] & Dkt. Deborah Amukowa[3]*

[1]Chuo Kikuu cha Kibabii, S.L.P 1699 – 50200, Bungoma, Kenya, muyundos@gmail.com.
[2]Chuo Kikuu cha Kibabii, S.L.P 1699 – 50200, Bungoma, Kenya, wsimiyu@kibu.ac.ke.
[3]Chuo Kikuu cha Kibabii, S.L.P 1699 – 50200, Bungoma, Kenya, dnanyama@yahoo.com.

**Article history:**

*Received: 19 Aug 2019*
*Accepted: 21 Aug 2019*
*Published: 23 Aug 2019*

**Keywords**:

*Masimulizi,*
*Mchakato,*
*Msuko,*
*Matukio,*
*Wahusika,*
*Maudhui*

## IKISIRI

Masimulizi katika mchakato wa ufundishaji wa vipengele maaalum vya msuko katika riwaya ya *Kidagaa Kimemwozea* na ile ya *Chozi la Heri.* Lengo la Makala haya lilikuwa ni kubainisha namna ambavyo masimulizi yalivyojitokeza katika mchakato wa ufundishaji wa kipengele maalum cha msuko katika riwaya ya *Kidagaa Kimemwozea* na ile ya *Chozi la Heri*. Utafiti huu ulitumia muundo wa kithamano mkabala wa kimfano. Mbinu za ukusanyaji data zilizotumiwa ni uchunzaji usaili na majadiliano ya vikundi viini. Data iliwasilishwa kwa kutumia maelezo ya kifafanuzi ,majedwali, nukuu za dondoo kutoka kwa mahojiano. Sampuli lengwa ilihusisha shule 10 kati ya 27, wasailiwa 18 kati ya 54 katika Kaunti ndogo ya Navakholo. Matokeo ni kwamba matukio yalitiririshwa katika mchakato wa ufundishaji wa vipengele maalum vya fani na maudhui katika riwaya ya *Kidagaa Kimemwozea* na ile ya *Chozi la Heri*.

## UTANGULIZI

Makala haya yalijadili masimulizi katika mchakato wa ufundishaji wa kipengele maalum cha msuko katika riwaya ya *Kidagaa Kimemwozoea* na ile ya *Chozi la Heri*. Fasihi katika lugha ya Kiswahili inafundishwa kwa viwango mbalimbali katika taifa la Kenya. Nchini Kenya, kwa mujibu Taasisi ya Ukuzaji Mitaala Kenya (TUMK - KICD) fasihi inafundishwa kama fasihi simulizi na fasihi andishi katika kiwango cha shule za upili. Fasihi andishi hugawika katika ushairi, tamthilia, hadithi fupi na riwaya. Hivyo basi, ni dhahiri kama anavyosema Oloo (2011), kwamba riwaya ya kiswahili hufundishwa katika kiwango cha shuke za upili kama mojawapo ya tanzu za fasihi kufundisha na kutahiniwa kwa riwaya ya *Kidagaa Kimemwozea* katika shule za upili katika mtihani wa KCSE ( *Kenya Certificate of Secondary Education*) kulianza mwaka wa 2013. Riwaya hii ilifundishwa na kutahiniwa hadi mwaka wa 2018. Kwa mujibu wa Taasisi ya Ukuzaji Mitaala Kenya (TUMK - KICD), wanafunzi katika kiwango cha shule ya upili wanapaswa kufundishwa riwaya moja ambayo watatahiniwa katika karatasi ya tatu. Mwaka wa 2018 wanafunzi wa kidato cha nne walitahiniwa riwaya ya *Kidagaa Kimemwozea* kwa mara ya mwisho na kuanzia mwaka wa 2019 riwaya ile ya *Chozi La Heri* itachukua pahala pake riwaya ya *Kidagaa Kimemwozea* katika utahini katika mtihani wa KCSE.

Kwa upande mwingine masimulizi yamerejelewa katika fasihi ya Kiswahili. Kwa mujibu wa Mwambi (2011) ambaye mojawapo ya matokeo yake yaliangalia jinsi masimulizi yalivyotumika katika tamthilia ya Kiswahili. Naye Washiali (2015) alirejelea usimulizi katika riwaya za; *Adili na Nduguze*, *Walenisi* na *Babu alipofufuka* kwa kuangalia jinsi masimulizi haya yalijitokeza katika riwaya kwa kufuata muundo maalum katika utunzi wake. Pia, Khamisi (2015) alishughulikia Uhakiki wa usimulizi katika tamthilia ya *Kijiba cha Moyo* na *Mstahiki Meya*. Hivyo basi makala haya yalijadili jinsi masimulizi yalivyojitokeza katika mchakato wa ufundishaji wa kipengele maalum cha msuko katika riwaya ya *Kidagaa Kimemwozoea* na ile ya *Chozi la Heri*.

## MBINU ZA UTAFITI

Utafiti huu ulitumia muundo wa kithamano mkabala wa kimfano. Mbinu za ukusanyaji data zilizotumiwa ni uchunzaji, usaili na majadiliano ya vikundi viini. Data iliwasilishwa kwa kutumia maelezo ya kifafanuzi majedwali, mifano na nukuu za dondoo kutoka kwa mahojiano au sehemu muhimu za kazi teule. Sampuli lengwa katika utafiti huu ilhusisha riwaya mbili (2) za Kiswahili riwaya ya *Kidagaa Kimemwozea* na ile ya *Chozi La Heri*. Jumla ya shule zote mbili (2) za wavulana, shuke moja (1) pekee ya wasichana na shule saba (7) kati ya ishirini na nne (24) za mseto zililegwa na utafiti huu. Shule hizi kumi (10) legwa kwa jumla kati ya shule ishirini na saba (27) ziliwakilisha asilimia thelathini na saba (37%) utafiti huu ulilenga kuhusisha wasailiwa kumi na nane (18) kati ya wasailiwa hamsini na nne (54) wa Kaunti hii ndogo ya Navakholo. Mbinu ya utabakishaji ilitumika kugawa shule kumi (10) katika daraja za shule za wavulana mbili (2) shule ya wasichana moja (1) na shule saba (7) za mseto. Vitabu viwili (2) riwaya ya *Kidagaa Kimemwozea* na ile ya *Chozi la Heri* vilichaguliwa kwa kurejelea kigezo cha riwaya hizi kutahiniwa katika kiwango cha shule za upili. Walimu kumi na nane (18) walichaguliwa kutumia mbinu ya usampulishaji wa kimaksudi. Mwalimu mmoja alilengwa kushiriki kwa kuchaguliwa kinasibu kwa usaili na majadiliano ya vikundi viini.

## MSINGI WA NADHARIA

Utafiti huu uliongozwa na Nadharia ya Naratolojia. Nadharia hii iliasisiwa na Gennette (1980). Kulingana na Bal (1997), ni nadharia inayorejelea masimulizi ya matukio na vitu vya kitamaduni ambavyo vinaeleza hadithi. Makala haya yalitumia mtazamo wa Bal (K.h.j) kwa kutumia mhimili ulioongoza utafiti ukiwa kutathmini namna ambavyo masimulizi ya mwalimu yalivyotumiwa katika mchakato wa ufundishaji wa kipengele cha msuko katika riwaya ya *Kidagaa Kimemwozea* na *Chozi la Heri.*

## MATOKEO YA UTAFITI

### Masimulizi katika mchakato wa ufundishaji wa kipengele cha msuko katika riwaya ya *Kidagaa Kimemwozea* na ile ya *Chozi la Heri*.

Sehemu hii ilishughulikia lengo la tatu la utafiti huu. Lengo hili lilikuwa Masimulizi katika mchakato wa ufundishaji wa kipengele cha msuko katika riwaya ya *Kidagaa Kimemwozea* na ile ya *Chozi la Heri*. Masimulizi yoyote yale ili yavutie na kueleweka msimulizi alihakikisha kuwa amepanga vitushi katika masimulizi yake kwa mpangilio ulioeleweka kwa urahisi. Msimulizi kwa kupanga vitushi hivi vya masimulizi huwa kwa mpangilio ulio na mantiki ili kurahisisha kueleweka kwa masimulizi yake kwa hadhira yake lengwa. Wasailiwa katika mchakato wa ufundishaji wa riwaya hizi za *Kidagaa Kimemwozea* na ile ya *Chozi la Heri*, vile vile walisimulia hoja zao kwa mpangilio mwema, kwa kuteua na kusimulia vitushi tofauti vya masimulizi yao kwa ufundi mkubwa.

Kipengele cha ploti kilikuwa mojawapo ya vipengele vya kimsingi vilivyorejelewa katika kufundisha kwa riwaya hizi za *Kidagaa Kimemwozea* na ile ya *Chozi la Heri*. Kipengele hiki kilirejelewa kwa wanafunzi kusoma riwaya hii darasani huku walimu wakiwaelekeza wanafunzi hawa katika kuchanganua kwa sehemu hizi baada ya kusoma sura baada ya sura. Wasailiwa walitumia misuko tofauti katika kufundisha kwa kipengele cha msuko katika riwaya hizi za *Kidagaa Kimemwozea* na ile ya *Chozi la Heri*. Misuko iliyobainika katika mchakato wa ufundishaji wa riwaya hizi mbili ilikuwa ni msuko sahili na msuko

changamano kama wanavyosema Mayieka (2015) na Oyoyo (2013). Misuko hii ilijitokeza katika mchakato wa ufundishaji wa riwaya hizi mbili kipengele hiki cha msuko kilipofundishwa kama ifuatavyo.

Lengo hili la tatu matokeo yake yalikusanywa kwa kuongozwa na nadharia ya Naratolojia iliyoasisiwa na Genette (1980). Nadharia hii ilitumia mhimili wa tatu uliokuwa uwepo wa mtiririko wa matukio katika masimulizi yanayosimuliwa na mwalimu katika ufundishaji wa riwaya hizi mbili kama ilivyoasisiwa na Bal (K.h.j). Nadharia hii ndiyo iliyokuwa dira ya matokeo ya utafiti wa lengo hili la tatu kama ifuatavyo:

**Msuko sahili**

Riwaya hizi za *Kidagaa Kimemwozea* na ile ya *Chozi la Heri* zilifundishwa na wasailiwa kwa kutumia misuko tofauti. Kwanza, wasailiwa walitumia msuko sahili. Kwa mujibu wake Oyoyo (K.h.j) msuko sahili huwa na matukio yanayotiririka kuanzia tukio la kwanza hadi tukio la mwisho. Wamitila (2003) alirejelea msuko huu sahili kama vile msuko wa msago. Katika aina hii ya msuko, wasailiwa hawa walisimulia matukio katika riwaya hizi kwa kuyafuatanisha kimantiki kutoka mwanzo hadi mwisho. Wasailiwa walisimulia kwa kujengana kwa vitushi kimasimulizi kwa kusimulia vitushi hivi moja kwa moja huku vikipangwa kuanzia cha kwanza hadi cha mwisho. Msuko huu ulipanga vitushi hivi jinsi vilivyokuzwa na kujengana katika masimulizi.

Msuko wa kwanza uliojitokeza katika mchakato wa ufundishaji wa riwaya ya *Chozi la Heri* uliotumiwa na wasailiwa ulikuwa msuko sahili. Kwa mujibu wa Oyoyo (K.h.j) katika aina hii ya msuko, katika mchakato wa ufundishaji wa kipengele hiki cha msuko msailiwa alirejelea vitushi tofauti na kuvipanga kwa njia ya vitushi hivi kuathiriana. Hali hii ilijitokeza kwa kurejelea nukuu ya mwalimu kutoka kwa kusoma kwa pamoja kwa sura ya pili katika riwaya ya *Chozi la Heri.* Kwa mfano;

"… Siku ya nne baada ya mapinduzi walibisha mlangoni na alipofunguliwa na Subira alisalimiwa kwa kofi kubwa. Wahuni hawa walimuuliza aliko mumewe Kaisari. Wahuni hawa walimkata Subira mikato miwili kwa sura akazirai kwa uchungu. Genge hili liliwabaka Lime na Mwanaheri na kuondoka. Tulia jirani yake aliwaita watoke nje na aliwasaidia katika kufunga virago vyao na kuwasindikiza hadi njia panda…"

Nukuu hii ilirejelea mwalimu katika mchakato wa ufundishaji wa riwaya hii ya *Chozi la Heri.* Masimulizi haya yalisimulia kipindi cha kusoma kwa sura ya pili katika riwaya hii. Msailiwa alielezea kwa kifupi msuko wa sehemu hii baada ya kusomwa kwa sehemu hii darasani. Msuko huu wa sura hii ya pili ulijitokeza kama ifuatavyo:

Masimulizi yalipangwa kwa kuanzia sehemu hii ya A iliyokuwa sehemu ya kwanza. Sehemu hii ilirejelea siku ya nne baada ya mapinduzi wahuni walipobisha mlangoni na ulipofunguliwa na Subira alisalimiwa kwa kofi kubwa. Hii ilifuatwa na sehemu ya B wahuni hawa wanapoulizia kuhusu aliko Kaisari mumewe wa Subira. Wahuni hawa walimkata Subira mikato miwili kwa sura akazirai kwa uchungu. Tukio hili lilifuatwa na sehemu ya tatu ya C pale genge hili liliwabaka Lime na Mwanaheri huku Kaisari akitazama na likaondoka. Hatimaye sehemu ya mwisho ni ile ya D Tulia jirani yake Kaisari anapokuja na aliwaita watoke nje kabla ya kuteketezwa ndani ya nyumba yao. Tulia aliwasaidia katika kufunga virago vyao na kuwasindikiza hadi njia panda.

Matukio katika nukuu hii yamepangwa kwa njia ya moja kwa moja kuanzia kwa tukioa la A hadi tukio la D. Msuko huu unaanza na kitendo cha kwanza ambacho ni kubisha kwa wahuni wale mlango hadi tukio la mwisho ambalo ni kuagana na jirani yao Tulia katika njia panda huku akiwahakikishia atawachungia mali yao. Nukuu hii ilifuata mpangilio wa sehemu A, sehemu B, sehemu C hadi sehemu D. Kwa mujibu wa Oyoo (K.h.j) msuko sahili ni msuko ambao hauna mrejelezi nyuma. Msuko huu ndio unaorejelewa kama msuko wa sahili. Matumizi ya msuko sahili yangekuwa mwafaka mno katika mchakato wa ufundishaji kwa vile yalieleweka kwa urahisi na yalimruhusu mwanafunzi kutabiri matukio yafuatayo hivyo kumvutia na kumchangamsha mwanafunzi.

Matokeo ya utafiti katika mchakato wa ufundishaji wa riwaya hizi *Kidagaa Kimemwozea* na ile ya *Chozi la Heri* yalikuwa kwamba wasailiwa walifundisha kwa kupanga matokeo yao katika msuko sahili. Hii ni kwa sababu walisoma sehemu fupi fupi kwa minajili ya wakati uliopo katika

ufundishaji huu. Wasailiwa wengi walifundisha fasihi kwa kipindi kimoja au vipindi viwili mtawalia katika kufundisha kwa riwaya hizi. Vipindi hivi vilikuwa ni vipindi vya dakika arubaini katika kila kipindi. Hivyo basi muda huu mfupi uliyafanya masimulizi mengi kuwa mafupi na hivyo matumizi ya msuko huu sahili kuwa mwafaka zaidi katika kufundisha kwa vipengele hivi viwili. Msuko huu sahili pia ulikuwa rahisi kueleweka kwa vile vitushi vya msuko vilipangwa kwa njia ya kuathiriana moja kwa moja na hivyo mwanafaunzi hakuhitajika kuunganisha vitushi kadhaa ili kupata maana. Usahili huu ulifanya msuko huu kuwa mwafaka haswa kwa wanafunzi wenye kiwango cha uelewa cha chini. Msuko sahili pia ulijitokeza sana kwa vile muundo wa riwaya hizi mbili za *Kidagaa Kimemwozea* na ile ya *Chozi la Heri* zilikuwa na muundo mwepesi katika kufundisha kwa kiwango hiki cha shule za upili.

Oyoyo (K.h.j), akirejelea Uhakiki wa fani katika ngano tano za Kiswahili, alipata kuwa ploti ya ngano nne kati ya tano ni sahili huku ploti hizi masimulizi yake yakitiririka kimfuatano. Hali hii ya msuko sahili kujitokeza katika ngano hizi tano ni kwa vile ngano ni tungo fupi hivyo ni rahisi kwa msuko sahili kutumika. Kuwepo kwa ploti hii katika ngano hizi za Kiswahili kama alivyopata Oyoyo (K.h.j) kulionyesha kuwa ploti sahili pia iliweza kutumika katika ufundishaji wa riwaya hizi za *Kidagaa Kimemwozea* na ile ya *Chozi la Heri*. Licha ya kuwa Oyoyo alirejelea uandishi wa ngano hizi tano. Utafiti huu umechangia kwa kuangalia kujitokeza kwa ploti sahili katika ufundishaji riwaya hizi mbili. Oyoyo (K.h.j) anasema kuwa matukio ya msuko sahili huondoa uwezekano wa kuwachosha wasikilizaji katika usimulizi wa ngano. Vile vile kama asemavyo Oyoyo (K.h.j) msuko sahili ni mwafaka kwa vile wasikilizaji wanaweza kutabiri kila tukio na hivyo masimulizi huvutia na kusisimua.

Matokeo ya utafiti katika mchakato wa ufundishaji wa riwaya hizi *Kidagaa Kimemwozea* na ile ya *Chozi la Heri* yalikuwa kwamba wasailiwa walifundisha kwa kupanga matokeo yao katika msuko sahili. Hii ni kwa sababu walisoma sehemu fupi fupi kwa minajili ya wakati uliopo katika ufundishaji huu. Matumizi ya msuko sahili yangekuwa mwafaka mno katika mchakato wa ufundishaji kwa vile yalieleweka kwa urahisi na yalimruhusu mwanafunzi kutabiri matukio yafuatayo hivyo kumvutia na kumchangamsha mwanafunzi. Vile vile msuko huu sahili ni mwafaka kwa vile wasikilizaji wanaweza kutabiri kila tukio na hivyo masimulizi huvutia na kusisimua. Riwaya hizi mbili zilizofundishwa katika kiwango hiki cha shule za upili zilikuwa na muundo mwepesi hivyo msuko sahili ulijitokeza katika ufundishaji wa riwaya hizi.

**Msuko Changamano**

Riwaya hizi za *Kidagaa Kimemwozea* na ile ya *Chozi la Heri* zilifundishwa na wasailiwa kwa kutumia msuko changamano. Oyoyo (K.h.j) anasema kuwa msuko changamano ni msuko ambao huhusisha matukio yale yakifuatana kiwakati na kiusababishi. Msuko huu changamano pia ulirejelewa na Oyoyo (K.h.j) kama msuko wa kioo. Msuko huu ulihusisha wasailiwa wakisimulia matukio kwa kurudia jambo lililokwisha kuelezwa na msailiwa katika riwaya hizi mbili kwa kutumia mbinu rejeshi kwa wingi kama anavyosema Oyoyo (K.h.j). Msuko huu uliashiriwa na matukio tofauti katika riwaya hizi mbili kudakiyana. Hivyo basi ni wazi kuwa msuko huu ulijengeka kwa mbinu rejeshi na kiangaza mbele katika ufundishaji wa riwaya ya *Kidagaa Kimemwozea* na ile ya *Chozi la Heri*.

Wasailiwa katika masimulizi yao ya kipengele cha ploti wakati mwingine walielezea matukio yaliyomalizia hadithi kama mwanzo, baada ya kuendelea na masimulizi huku kisa kikielezwa baadaye kidogo. Wasailiwa waliendelea na masimulizi yao na walipofika mwisho wa masimulizi, walirudia tena kueleza yale matukio yaliyoelezwa mwanzo katika riwaya hizi za *Kidagaa Kimemwozea* na ile ya *Chozi la Heri*. Msuko huu hurejelewa kama mbinu rejeshi au kisengere nyuma ilipotumika na wasailiwa shuleni.

Kipengele hiki cha msuko pia kilijitokeza katika kipindi cha kusoma kwa riwaya hii ya *Kidagaa Kimemwozea*. Msailiwa alipowafundisha wanafunzi hawa riwaya hii ilisomwa darasani huku mwalimu akiwaelekeza katika kujadili msuko. Dondoo hii ya msailiwa ilirejelea msuko changamano. Hali hii ilijitokeza kwa kurejelea nukuu kutoka kwa kusoma kwa pamoja kwa sura ya

kumi katika riwaya ya *Kidagaa Kimemwozea*. Kwa mfano:

"…Mtemi Nasaba Bora alipotea na kuwacha gari lake limeegeshwa karibu na jumba la Majununi. Amani aliishi kwenye kijijumba cha wafanyikazi cha Mwalimu Majisifu anachomtembelea ili wawe na mazungumzo marefu na Amani. Mwalimu Majisifu alimweleza Amani kuwa usiku wa kuamka juzi Mtemi Nasaba Bora alikuja kumpa buriani. Mtemi aliungama dhambi kwa Amani kwa vile aliandika barua ndefu yenye maelezo ya kumwondoa lawamani amu Yusufu kwa kuitia sahihi.

Nukuu hii ilirejelea msailiwa katika mchakato wa ufundishaji wa riwaya hii ya *Kidagaa Kimemwozea*. Masimulizi haya yalisimulia matukio katika sura ya kumi katika riwaya hii baada ya wanafunzi kusoma kwa pamoja. Msailiwa alielezea kwa kifupi msuko wa sehemu hii baada ya kusomwa kwa sehemu hii na wanafunzi darasani kwa pamoja. Msuko huu katika sura hii katika masimulizi ulijitokeza kama ifuatavyo:

Msuko wa vitushi wa nukuu hii ya msailiwa ulikuwa nguzo muhimu katika ufundishaji wa kipengele hiki. Sehemu ya kwanza katika masimulizi haya ya msailiwa ilikuwa sehemu ya C. Sehemu hii ilirejelea kitendo cha Mtemi Nasaba Bora kupotea na kuliwacha gari lake likiwa limeegeshwa karibu na jumba la Majununi. Hii ilifuatwa na sehemu ya D iliyohusisha Amani aliyeishi kwenye kijijumba cha wafanyikazi cha Mwalimu Majisifu anachomtembelea ili wawe na mazungumzo marefu naye. Sehemu ya A ilikuwa ni ya tatu hapa mbinu rejeshi ikijitokeza na Mwalimu Majisifu alimweleza Amani kuwa usiku wa kuamka juzi Mtemi Nasaba Bora alikuja kumpa buriani baada ya kutamauka na maisha kwa kuozewa kidagaa. Mbinu rejeshi iliendelea Sehemu ya B ilimrejelea Mtemi alipoungama dhambi kwa Amani kwa vile aliandika barua ndefu yenye maelezo ya kumwondoa lawamani amu Yusufu kwa kuitia sahihi. Msuko wa vitushi katika nukuu hii kwa mujibu wa Oyoyo (K.h.j) ni msuko changamano. Msuko huu ulianza na sehemu ya C na kukamilika kwa sehemu ya B. Msuko wa vitushi hivi ulikuwa sehemu C, sehemu D, sehemu A na kukamilika kwa D.

Msuko changamano ulijitokeza katika mchakato huu wa ufundishaji wa ploti katika riwaya hizi za *Kidagaa Kimemwozea* na ile ya *Chozi la Heri*. Hali hii ilitokana na hali ya msimulizi kurejelea masimulizi yaliyosheheni mbinu rejeshi na kiangaza mbele. Hii ilitokana na msailiwa kurejelea visa viwili, kisa cha Mtemi Nasaba Bora na kile cha Amani katika riwaya ya *Kidagaa Kimemwozea*. Kisa chake Mtemi kikiwa kisa kikuu nacho cha Amani kikitumiwa kurejelea cha Mtemi. Msuko huu changamano katika kufundisha kwa ploti katika riwaya hizi za *Kidagaa Kimemwozea* na *Chozi la heri* ulipotumiwa wasailiwa walihisi kuwa huenda wanafunzi wasielewe haraka msuko huu. Hii ni kwa sababu msuko huu ulikuwa mwafaka kwa masimulizi marefu. Hata hivyo masimulizi mengi ya wasailiwa yalikuwa mafupi na hivyo masimulizi ya msuko changamano yalikuwa machache katika ufundishaji. Hali hii ni muhimu katika ufundishaji wa riwaya hizi kwa vile kwa mwalimu kutumia msuko changamano wanafunzi huenda wakachoshwa na masimulizi yale. Kwa masimulizi yale kuwa marefu wanafunzi walipoteza nathari yao haraka kwa masimulizi haya kwa kuchoshwa na masimulizi haya. Wanafunzi wa uelewa wa kiwango cha chini pia walikuwa na shida katika kuelewa masimulizi changamano katika kufundisha kwa riwaya hizi mbili. Hivyo basi msuko huu haukuwa mwafaka kwa wanafunzi wa kiwango cha chini cha uelewa katika kufundisha kwa riwaya hizi.

Oyoyo (K.h.j) katika kuhakiki mighani ya Fumo Liyongo msuko unaojitokeza ni msuko changamano. Msuko huu ulitokana na mvutano kati ya Liyongo na ndugu yake Daudi Mringwari kurejelea urithi wa ufalme unaufanya msuko wa hadithi kuwa changamano na wenye mvuto kwa matumizi mengi ya mbinu ya taharuki. Hivyo basi ni dhahiri kuwa msuko changamano ulijitokeza katika ngano za Kiswahili. Hii ilikuwa muhimu kwa vile ilidhihirisha kuwa masimulizi yaliweza kutumiwa pia katika ufundishaji wa riwaya ya Kiswahili. Utafiti huu pia ulipata kuwa msuko changamano ulitumika katika ufundishaji wa riwaya hizi za *Kidagaa Kimemwozea* na *Chozi la Heri*.

Burundi na wenzake (2007) pia walipata ploti hii changamano katika uchunguzi wao wa usimulizi katika *Utenzi wa Swifa ya Nguvumali*. Msuko huu

changamano kwa kujitokeza kwa uandishi wa *Utenzi wa Swifa ya Nguvumali* ni idhibati tosha kuwa unaweza kutumiwa katika ufundishaji wa riwaya ya Kiswahili. Hili ni dhahiri kutokana na matokeo ya awali msuko huu changamano ulipojitokeza katika ufundishaji wa riwaya hizi za *Kidagaa Kimemwozea* na *Chozi la Heri*.

Msuko changamano ulijitokeza katika mchakato huu wa ufundishaji wa ploti katika riwaya hizi za *Kidagaa Kimemwozea* na ile ya *Chozi la Heri*. Hali hii ilitokana na hali ya msimulizi kurejelea masimulizi yaliyosheheni mbinu rejeshi na kiangaza mbele. Hii ilitokana na msailiwa kurejelea visa viwili, kisa cha Mtemi Nasaba Bora na kile cha Amani katika riwaya ya *Kidagaa Kimemwozea*. Kisa chake Mtemi kikiwa kisa kikuu nacho cha Amani kikitumiwa kurejelea cha Mtemi. Hata hivyo msuko huu changamano ulipotumiwa na wasailiwa katika kufundisha riwaya hizi wanafunzi walichoka haraka kutokana na urefu wa masimulizi yale na uchangamano wake. Wanafunzi wa kiwango cha chini cha uelewa pia walitatizika kutokana na urefu na uchangamano wa masimulizi yao, hii ni kwa sababu matukio hayakupangwa kwa njia ya moja kwa moja na walihitajika kuhusisha matukio yaliyosukwa kwa mpangilio uliovurugika.

Kimsingi, katika kufundisha kwa riwaya hizi za *Kidagaa Kimemwozea* na ile ya *Chozi la Heri*, wasailiwa walipanga misuko ya masimulizi yao kwa njia yoyote ile ilimradi waafikie malengo yao ya ufundishaji wa riwaya ya *Kidagaa Kimemwozea* na ile ya *Chozi la Heri*. Wasailiwa walipofundisha riwaya hizi katika masimulizi yao si lazima walirejelea matukio tofauti katika masimulizi yao pale darasani.

Hivyo basi ilidhihirika wazi kuwa misuko yote miwili ilijitokeza katika ufundishaji wa riwaya hizi mbili za *Kidagaa Kimemwozea* na ile ya *Chozi la Heri* katika kufundisha kwa kipengele hiki cha ploti. Matumizi ya msuko sahili yangekuwa mwafaka mno katika mchakato wa ufundishaji kwa vile yalieleweka kwa urahisi na yalimruhusu mwanafunzi kutabiri matukio yafuatayo hivyo kumvutia na kumchangamsha mwanafunzi.

## HITIMISHO

Matokeo ya utafiti huu yalikuwa katika kufundisha kwa riwaya hizi za *Kidagaa Kimemwozea* na ile ya *Chozi la Heri* masimulizi yalijitokeza katika mchakato wa ufundishaji wa kipengele hiki cha msuko. Msuko sahili na msuko changamano ulitumika katika kutiririsha vitushi katika masimulizi kwa mchakato wa kufundisha kwa riwaya hizi za *Kidagaa Kimemwozea* na ile ya *Chozi la Heri*.

## MAPENDEKEZO

Haja ipo ya utafiti kufanywa kwa kurejelea riwaya nyinginezo sio tu riwaya hizi za *Kidagaa Kimemwozea* na ile ya *Chozi la Heri*. Vile vile utafiti ufanywe kwa tanzu nyinginezo za fasihi andishi kama vile hadithi fupi na tamthilia wala sio riwaya pekee. Hatimaye utafiti ufanywe kwa kurejelea vipengele mahususi vya fani au maudhui wala sio vyote kwa jumla.

## MAREJELEO


Bal, M. (1997). *Introduction to the theory of Narrative*. University of Toronto Press.

Burundi, N.R., Mukuthuria, M. na Matundura E.S. (2007). ‘Usimulizi katika Utenzi wa Swifa ya Nguvumali. Katika Nordic Journal of African Studies 16 (3) uk. 73-86.

Genette, G. (1980). *Narrative Discourse : An Essay in Method.*Cornell University Press.

Khamisi, S.B. (2015) Uhakiki wa usimulizi katika tamthilia ya *Kijiba cha Moyo* na *Mstahiki Meya*. Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Nairobi. Haijachapishwa.

Mayieka, M.N. (2015). Masuala ibuka katika riwaya za kisasa ; *Kidagaa Kimemwozea* na *Mhanga nafsi yangu*. Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Kenyatta. Hajachapishwa.

Mwambi, P. (2011). Matumizi na malumbano katika tamthilia ya Kiswahili. Chuo Kikuu cha Kenyatta. Tasnifu ya Uzamili. Hajachapishwa.

Oloo, O.A. (2011). Tathmini ya Matumizi ya TEKNOHAMA katika Ufundishaji waRiwaya

ya Kiswahili katika Shule za Upili Kaunti ndogo Kisumu Magharibi. Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Masinde Muliro cha Sayensi na Teknolojia. (Haijachapishwa)

Oyoyo, O.J. (2013) Uhakiki wa fani katika ngano tano za Kiswahili. Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa)

Wamitila, K.W. (2008) *Kanzi ya Fasihi 1: Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi.* Nairobi. VideMuwa Publishers Limited.

___________ (2003 B) *Kichocheo cha Fasihi Simulizi na Andishi*. Nairobi: Focus Books.

Washiali, O. C. (2015). Usimulizi katika riwaya za; *Adili na nduguze*, *Walenisi* na *Babu Alipofufuka*. Chuo Kikuu cha Kenyatta. Tasnifu ya Uzamili. Haijachapishwa.